

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA KUMI NA MBILI**

**KIKAO CHA NANE**

**07 SEPTEMBER, 2023**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

### MKUTANO WA KUMI NA MBILI

**KIKAO CHA NANE – TAREHE 07 SEPTEMBER, 2023**

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA FEDHA:**

Maelezo ya Waziri wa Fedha kuhusu Muswada wa Sheria ya Ununuzi wa Umma wa Mwaka 2023.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Muswada wa Sheria ya Ununuzi wa Umma wa Mwaka 2023.

### **III. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:**

### **IV. MASWALI YA KAWAIDA:**

#### **OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

#### **112. MHESHIMIWA MICHAEL MWITA KEMBAKI (TARIME MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Shule ya Bweni ya Wasichana Tarime Mjini.

#### **113. MHESHIMIWA GEORGE NATANY MALIMA (MPWAPWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Vituo vya Afya katika Kata za Mlembule, Godegode, Chunyu na Berege - Mpwapwa.

#### **114. MHESHIMIWA KASSIM HASSAN HAJI (MWANAKWEREKWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Sheria ya Mfuko wa Jimbo itarekebishwa kuondoa kikwazo cha utekelezaji Zanzibar kwa kuwa Wabunge siyo Madiwani.

**OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):**

**115. MHESHIMIWA AIDA JOSEPH KHENANI  
(NKASI KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, kuna mpango gani wa kutoa Semina elekezi mara kwa mara kwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya kuhusu Utawala Bora.

**WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA  
TEKNOLOJIA YA HABARI:**

**116. MHESHIMIWA MARGARET SIMWANZA  
SITTA (URAMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, lini Serikali itapeleka mawasiliano ya simu Wilaya ya Urambo katika maeneo ambayo orodha yake iliwasilishwa Wizarani.

## **WIZARA YA UJENZI:**

### **117. MHESHIMIWA ABDALLAH JAFARI CHAUREMBO (MBAGALA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, kuna mpango gani wa kujenga mifereji Barabara ya Kigamboni – Kongowe, Mtaa wa Mikwambe, Kata ya Toangoma - Mbagala.

## **WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

### **118. MHESHIMIWA MWANAKHAMIS KASSIM SAID (MAGOMENI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, kwa nini Jeshi la Polisi haliondoi zuio la kuwahudumia Wananchi wanaokwenda kupata huduma kwenye Vituo nje ya maeneo yao.

### **119. MHESHIMIWA FAKHARIA SHOMAR KHAMIS (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lipi tamko la Serikali kwa Watuhumiwa waliopo Magereza ya Nchi za Nje wanaomiliki Vitambulisho na Hati za Kusafiria za Tanzania.

## **WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:**

### **120. MHESHIMIWA ZACHARIA PAULO ISSAAY (MBULU MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Jengo la Mahakama Wilayani Mbulu.

### **121. MHESHIMIWA TECLA MOHAMED UNGELE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, lini Serikali itajenga Jengo jipya la Mahakama ya Wilaya Nachingwea.

## **V. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:**

***(Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge Zima  
na Kusomwa Mara ya Tatu)***

Muswada wa Sheria ya Ununuzi wa Umma wa Mwaka 2023.

**DODOMA  
07 SEPTEMBER, 2023**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*  
KATIBU WA BUNGE**